# Uchambuzi wa Dhima ya Msimulizi katika Bunilizi ya Watoto ya *Zindera* (2008)

Elizabeth G. Mahenge
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kuchambua dhima za msimulizi wa hadithi ya ualbino katika bunilizi ya watoto ya *Zindera* (2008). Msimulizi wa kazi hii anasawiri mitazamo miwili iliyopo katika jamii kuhusu watu wenye ualbino, mitazamo ambayo kwa namna fulani inaelekeana japokuwa inatofautiana. Mtazamo wa kwanza ni wa kizamani ambao unadhihirishwa na watu wa jamii ya Zindera ambao wanawaua watoto wenye ualbino ili kuondoa mikosi, majanga na vifo katika jamii. Mtazamo wa pili unahusisha mauaji au ukataji wa viungo vya watu wenye ualbino kwa ajili ya kutafuta utajiri na kupanda cheo. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Naratolojia ambayo kwa mujibu wa Bal (2008) inahusu usimulizi wa hadithi. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa msimulizi amejitokeza katika dhima ya usimulizi, mawasiliano, ukosoaji na itikadi. Dhima hizi si ngeni katika fasihi mbalimbali duniani kwani pia zinajitokeza katika fasihi za Wamarekani na Waingereza kwa kutaja kwa uchache.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inahusu uchambuzi wa bunilizi ya watoto inayoitwa *Zindera* (2008) ili kujua dhima za msimulizi ambazo zinajitokeza katika kitabu hicho. Lengo la makala hii ni kuchambua dhima za msimulizi anayesimulia hadithi ya ualbino katika kazi hii. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Naratolojia ambayo inahusika na usimulizi wa hadithi. Tumegawa makala hii katika sehemu kuu tatu ambazo ni utangulizi, kiini na hitimisho. Utangulizi unatupatia muhtasari wa kazi inayochambuliwa pamoja na ufafanuzi kuhusu nadharia inayotuongoza katika uchambuzi wa data; na katika kiini tumeelezea namna msimulizi anavyojitokeza kupitia dhima mbalimbali katika kitabu teule. Mwisho tumetoa hitimisho la makala pamoja na mapendekezo.

## 2.0 Muhtasari wa Bunilizi ya Watoto ya *Zindera*

*Zindera* ni bunilizi ya watoto iliyotungwa na Erasto Gervas Sabuni na kuchapishwa mwaka 2008. Hii ni bunilizi inayomhusu mtoto mwenye ualbino ambaye baada ya kuzaliwa, mama yake anatakiwa amuue kwa sababu ya shinikizo la mila na desturi za jamii yake ili aondoe mikosi katika familia na ukoo. Mama yake anapinga uamuzi huo na anaamua kutorokea mbali asikokujua. Anamficha Zindera msituni baada ya kuhisi kuwa anafuatiliwa na mume wake. Kisha Zindera anaokotwa na kulelewa katika familia mpya. Anapofika darasa la sita, nyumba yao inaungua na walezi wake Bwana na Bibi Makale wanafariki. Zindera ananusurika kuuawa na waganga wa jadi ili kuchukua viungo vyake vikatumike kutengenezea dawa za kichawi za kuwapatia watu utajiri pamoja na kupanda vyeo kazini. Kutokana na tamaa hiyo ya Bitele na wateja wake, wanawekewa mtego na wananaswa kutokana na kumfanyia Zindera njama za kumwua; lakini Zindera anafanikiwa kutoroka na kuokolewa na maafande wa Jeshi la Polisi. Anapata familia mpya na kulelewa katika familia ya Afande Pita. Hatimaye anahitimu masomo yake na kuwa tabibu. Zindera anaajiriwa kama tabibu katika hospitali iliyopo kwenye kijiji chao na anafanikiwa kuwatibu wagonjwa mbalimbali akiwamo baba yake mzazi mzee Mpanduji, ambaye alitaka kumuua akingali mtoto mchanga wa siku moja, kutokana na imani potofu kuhusu ualbino.

## 3.0 Nadharia ya Naratolojia

Kwa mujibu wa Bal (1997), nadharia hii inatazama kila tendo la kisanaa, au fikra iliyowekwa katika maandishi, uchongaji vinyago, usanifu wa majengo, michoro, utarizi na ufinyanzi kama matukio yenye kusimulia jambo mahususi. Altman (2008) anashadidia hoja hii ya Bal kwa kusema kuwa usimulizi ni kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Tunaweza kuuona usimulizi kupitia vipengele kadhaa kama vile: utamaduni, njia ya kupashana habari na pia kupitia kushirikishana uzoefu mbalimbali wanaoupitia watu mbalimbali katika maisha yao. Kwa mujibu wa Altman (2008) vipengele hivi vinatupa usimulizi fulani ili kukamilisha maisha ya mwanadamu na kwamba, huwezi kuyatenga maisha ya mwanadamu na usimulizi. Kutokana na maelezo hayo ya Altman tunaweza kusema kwamba, maisha ya mwanadamu na usimulizi ni kama *pande mbili za sarafu moja*. Msemo huu unamaanisha kwamba huwezi kuwa na usimulizi bila kuwa na maisha na huwezi kuwa na maisha bila ya kuwa na usimulizi.

Kwa hivyo, ili maisha yapate maana yake kunahitajika kuwapo na usimulizi ambao unabadilika kimaumbo. Usimulizi unabadilika kimaumbo kulingana na maendeleo mbalimbali yanayojitokeza duniani ikimaanisha maendeleo ya kiteknolojia. Hii ni kwa kuwa usimulizi hapo kale ulianzia kwa njia ya mdomo na kumlenga msikilizaji au mtazamaji, kisha usimulizi ulihamishiwa kwenye njia ya maandishi na kumlenga mwandishi na msomaji. Baada ya hapo usimulizi ukahamia kwenye njia ya filamu ukimlenga mwigizaji kwa upande mmoja na mtazamaji au msikilizaji kwa upande mwingine. Katika miktadha yote hii ya mabadiliko ya kimaumbo ya uwasilishaji wa hadithi, usimulizi umeendelea kuwapo katika kila umbo (Altman, 2008). Mtaalamu mwingine ni Walsh (1997) ambaye anaelezea maana ya msimulizi kuwa ni mhusika ndani ya hadithi, ambaye husimulia hadithi ambayo anaweza kujihusisha nayo au asijihusishe nayo. Kauli hii ina maana kuwa akijihusisha nayo yeye si mtazamishaji lakini asipojihusisha nayo anakuwa ni mtazamishaji.

Kwa upande mwingine, Madumulla (2009) anafasili usimulizi au "…usimuliaji ni njia kuu ya mtunzi wa riwaya kudhibiti na kujenga maudhui yake. Usimuliaji huelekeza ujenzi wa wahusika, matukio na kila kitu kinachowakilishwa katika riwaya" (Madumulla, 2009:117). Hoja hii ya Madumulla (2009) imetuwezesha kuelewa maana ya msimulizi na hivyo itatuwezesha kufanya uchambuzi wa dhima za msimulizi katika kitabu teule ili tufahamu msimulizi anaibua kitu gani kinachohusiana na uumbaji wa ualbino, kupitia katika wahusika aliowaumba na anaowatumia pamoja na matukio yanayowazunguka.

Bal (1997) anakwenda mbele zaidi na kutueleza kuhusu ni nani anayefanya usimulizi katika kazi za kisanaa ambazo ziko katika maandishi. Masimulizi hayo hufanywa na wahusika – yaani wasimuliaji au watendaji wa hadithi (msimulizi wa ndani) ambao hutenda kwa lengo maalumu. Mwandishi huwatumia wasimulizi mbalimbali ili kuisimulia hadithi. Mwandishi huwafanya wahusika wake waongee na kusimulia kwa niaba yake. Kupitia kwa wakala, mwandishi hujitoa na kuwaacha wasimuliaji waelezee kisa kwa niaba yake kwa namna fulani inayoitwa *fabula*. Hivyo, mwandishi humtumia wakala ili kuisimulia hadithi. Katika nadharia hii, msimulizi ni wakala wa mwandishi. Wakala huyu anaweza kujibainisha katika madarajia mawili: darajia la kwanza ni lile linalotumia nafsi ya kwanza au ya pili; na darajia la pili ni linalotumia nafsi ya tatu. Madarajia haya yana maana yake kifasihi – kuunga mkono hoja na kupinga mkono hoja mtawalia.

Lengo kuu katika Nadharia ya Naratolojia ni kuchunguza muundo wa simulizi na sifa pambanuzi za msingi ambazo zinaipa umbo simulizi na ndicho kinachoitofautisha simulizi na miundo mingine. Mathalani, matumizi ya nafsi mbalimbali za usimulizi huweza kubaini hasa msemaji wa tukio fulani ni nani, na ana nafasi gani katika jamii. Kupitia katika nadharia hii tunaweza kugundua msimulizi ni nani. Tunaweza kuona wasemaji au watendaji wengine (wakala) nyuma yake ambao ndio wenye kauli kuhusu lile linalosemwa, na sio yeye mwenyewe. Katika muktadha huu, kuna msimulizi hai kwenye simulizi husika na msimulizi tuli. Kuwa 'hai' kwa msimulizi maana yake ni kwamba uhusika wake ni wa kiutendaji zaidi; na kuwa 'tuli' kwa msimulizi maana yake ni kwamba uhusika wake siyo wa kiutendaji. Kwa msimulizi kuwa mtendaji au la, kunatusaidia kuchanganua maana za kauli mbalimbali zinazotolewa na msimulizi. Msimulizi mtendaji ni yule mhusika anayepewa majukumu katika kusimulia hadithi na anajipambanua kwa kutumia nafsi ya kwanza na ya pili. Vivyo hivyo msimulizi asiye mtendaji ni yule anayejipambanua kwa kutumia nafsi ya tatu ya usimulizi. Nadharia ya Naratolojia imetuongoza katika kuelewa, kuchambua na kutathmini usimulizi kuhusu ualbino kama unavyojitokeza katika bunilizi ya watoto ya *Zindera*. Aidha, kipengele cha dhima za msimulizi kimetusaidia kuelewa au kuchambua namna msimulizi anavyoshika nyadhifa mbalimbali katika kusimulia hadithi ya ualbino katika kazi teule inayohusika.

Nadharia ya Naratolojia inatusaidia kufahamu namna ambavyo msimulizi anaingia katika fikra za wahusika wake na kisha tukaelezwa hata kile mhusika anachokikumbuka (Mohochi, 2000). Mbinu hii inamfanya msimulizi aingilie kati kila tukio kwa kuwaambia wasomaji kile kinachoendelea kwenye hadithi badala ya kuwaachia wasomaji nafasi ya kutafakari na kujiamulia wenyewe (Mohochi, 2000). Haya hufanyika kwa msimulizi kutoa maoni yake kuhusu jambo aliloliibua katika kazi husika ya kifasihi. Msimulizi pia anaweza kuwa mtazamishaji endapo anajitokeza hivyo katika simulizi husika kwa maana siyo mtendaji wa hadithi bali ni mtazamaji anayesimulia. Aidha, si kila msimulizi ni mtazamishaji. Kinaratolojia msimulizi na mtazamishaji ni viumbe tofauti.

## 4.0 Dhima za Msimulizi wa Hadithi kwa Mujibu wa Nadharia ya Naratolojia

Dhima ya msimulizi katika hadithi ni kazi ambayo inafanywa na wakala anayesimulia hadithi. Katika fasihi, dhima ya mwandishi ni pamoja na kuonya, kufundisha na kuadabisha jamii kwa kuzitaja kwa uchache. Tunapozungumzia dhima za msimulizi tunalenga kitu kilekile lakini tofauti yake ni kwamba, katika

muktadha huu wa usimulizi wa kinaratolojia, hatumzungumzii mwandishi bali msimulizi, yaani wakala wa mwandishi ambaye ameachiwa hadithi ili aisimulie kwa niaba ya mwandishi (mtunzi).

Bonn (2018) akielezea dhima ya msimulizi katika riwaya ya Kimarekani anakiri kwamba, msimulizi hujitokeza ili kutekeleza dhima mbalimbali katika bunilizi kama ilivyo katika maisha yetu ya kila siku ambapo, mtu mmoja hawezi kujua kila kitu kuhusu kila jambo linalotokea. Hivyo huwahitaji watu wengine wamjuze mtu huyu kuhusu jambo fulani. Vivyo hivyo, katika simulizi, msimulizi hawezi kuwa mwaminifu katika simulizi husika kwa kusimulia yeye mwenyewe; anahitaji kutekeleza dhima mbalimbali ili aweze kuaminika.

Wataalamu wa Nadharia ya Naratolojia wanaeleza kuwa msimulizi katika kusimulia hadithi anatekeleza dhima mbalimbali. Kwa mujibu wa Gennete (1980), msimulizi ana dhima tano ambazo ni kusimulia hadithi, kukosoa, kuwasiliana, kutoa ushuhuda na kuelezea itikadi. Katika dhima ya kwanza msimulizi anaiwezesha hadhira (wasomaji) kujua kinachoendelea katika hadithi hiyo. Dhima hii ya kusimulia inaweza kufanywa na msimulizi ambaye anajinasibisha na simulizi, kwa maana anazungumza kwa nafsi ya kwanza. Msimulizi akitumia nafsi ya kwanza inaonesha yuko hai inamaanisha anatimiza jukumu la kusimulia (Tendler, 2017). Pia, msimulizi anaweza kufanya simulizi kwa kutojinasibisha na simulizi, yaani anajitenga na kuwa mtazamaji. Ili aweze kutimiza jambo hilo la kujitenga katika simulizi, anatumia nafsi ya tatu (Gennete, 1980). Msimulizi akitumia nafsi ya tatu katika usimulizi maana yake hayuko hai katika kutimiza jukumu la kusimulia (Tendler, 2017). Mawazo ya Tendler ni sahihi kwa kiasi fulani kwani kulingana na utafiti wa Mahenge (2019) uhai au ufu (kutokuwa hai kiusimulizi) wa msimulizi ni jambo linaloifungamanisha simulizi na nafsi inayosimulia, kama ni nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu.

Dhima ya pili ni kukosoa. Katika dhima hii, msimulizi anaingilia kati kwenye simulizi na kutoa maoni yake ya kiukosoaji anapotekeleza namna jambo linavyotakiwa liwe, tofauti na lilivyofanywa na mhusika. Msimulizi akiingilia simulizi na kutoa maoni yake (kwa nafsi ya kwanza au ya pili), inamaanisha amejinasibisha na simulizi. Hii ni kwa sababu anachukua uhusika katika simulizi kama mhusika katika hadithi (Gennete, 1980; Fludernik, 2006; Hubert, 2016). Msimulizi anakuwa mhusika mtendaji kwa sababu ya kusimulia au kutoa maoni yake kwa kutumia nafsi ya pili.

Dhima ya tatu ni kuwasiliana. Katika dhima hii, msimulizi anazungumza moja kwa moja na msomaji ili kumfanya ahisi kuwa yeye ni sehemu ya simulizi,

na anatakiwa atimize majukumu fulani katika hadithi. Dhima hii hujitokeza kwa matumizi ya nafsi ya pili (Gennete, 1980; Fludernik, 2006; Hubert, 2016).

Dhima ya nne ni kutoa ushuhuda. Lengo la dhima hii ni kushadidia ukweli wa tukio fulani. Katika dhima hii, msimulizi anaweza kuelezea hisia zake kuhusu jambo husika linalosimuliwa kwa kuwa anakuwa ni shuhuda wa tukio hilo (Hubert, 2016).

Dhima ya tano ni ya kiitikadi. Dhima hii inamaanisha kuwa, msimulizi anafanya kazi ya kusimamia maadili ya jamii kwa kuelezea maadili mema au mawazo ya busara ambayo yanakusudiwa yawafikie wasomaji (Gennete, 1980; Fludernik, 2006; Hubert, 2016).

Mtaalamu mwingine aliyezungumzia dhima za msimulizi katika simulizi ni Phelan (2007) ambaye anataja aina tatu za dhima ambazo ni: kuripoti, kuelezea na kutathmini. Katika maelezo ya mtaalamu huyu, japokuwa ametumia istilahi tofauti, lakini ukizitazama dhima hizo kwa namna alivyozieleza zinaingiliana na zilezile za Gennete (1980), yaani kusimulia, kukosoa, kuwasiliana, kutoa ushuhuda na kueleza itikadi.

## 5.0 Dhima za Msimulizi katika Bunilizi ya Watoto ya *Zindera*

Katika bunilizi hii, msimulizi amebainika kuwa na dhima kadhaa. Dhima hizo ni: kukosoa, kueleza itikadi, kusimulia na kuwasiliana kama ambavyo inaelezwa katika sehemu inayofuata.

### 5.1 Kukosoa

Kukosoa ni suala lisiloweza kukwepeka katika maisha ya mwanadamu. Kukosoa au kukosolewa ni hali inayotokana na kutofautiana kwa mitazamo kati ya watu wa pande mbili ambapo, upande mmoja unaona hivi na upande mwingine unaona vile. Dhima ya kukosoa katika kazi za fasihi imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali wakiwamo Fludernik (2006) na Hubert (2016). Katika utafiti wetu, dhima ya msimulizi kama mkosoaji imejitokeza kupitia mila mbalimbali zinazohusishwa na watu wenye ualbino. Msimulizi katika bunilizi ya *Zindera*, anatueleza kuhusu mazungumzo kati ya wachungaji wawili. Wachungaji hawa walikuwa wanasimuliana kuhusu habari mbalimbali walizozisikia kuhusu watu wenye ualbino na imani mbalimbali wanazozisikia katika jamii zao. Wachungaji hawa wanapata mashaka kuhusu mambo yanayoelezwa kupitia imani hizo. Msimulizi anajitokeza katika dhima ya kukosoa mawazo ya wanajamii wanaoamini kuwa wanaweza kuwa matajiri kwa njia ya kishirikina. Kukosoa

huku kunajitokeza pale anaposema, "…kwa nini mganga wa kienyeji asianze kuwa yeye tajiri?" (Sabuni, 2008:12). Kauli hii ya mchungaji inaonesha jinsi msimulizi anavyokosoa tabia ya watu wasioweza kuchanganua mambo ambayo wanayaona katika jamii.

Mambo haya ni hali ya kimaisha ya mganga ambaye anamtuma Mage kuua watu wenye ualbino ili atajirike wakati mganga mwenyewe ana umaskini wa kutupwa. Kwa hiyo, msimulizi anamhusisha msomaji kushiriki katika mazungumzo (kwa sababu anazungumza naye huku akimuuliza maswali kuhusu tabia hii ya baadhi ya watu katika jamii. Dhima ya msimulizi katika muktadha huu ni hai kutokana na kutimiza majukumu katika kusimulia jambo hili. Pia ukosoaji unaendelea kuhusu uwezo wa kiakili wa hao watu ambao wameamini kuwa wanaweza kuwa matajiri kwa njia ya kishirikina. Ukosoaji huu unatendeka kupitia msimulizi mtendaji (anayetumia nafsi ya pili) kutokana na msimulizi kuuvaa uhusika wa mchungaji na kusema: "…wajinga ndio waliwao" (Sabuni, 2008:12) akimaanisha kuwa watu wenye akili na hekima hawawezi kukubali kudanganywa kwa kuambiwa kuwa wanaweza kutajirika kwa njia za kishirikina; badala yake, watu hao wenye akili wanafahamu njia halali zinazomwezesha mtu kutajirika. Lakini kwa wale walio "wajinga" wao hukubali kudanganyika na kulaghaiwa. Msimulizi anatumia msemo huu ili kushadidia mawazo yake kwamba *wajinga ndio waliwao*.

Ukosoaji mwingine unajitokeza pale mchungaji wa awali anapomkumbusha mwenzake kuhusu kuheshimu mila za jamii yao. Msimulizi katika dhima hii anajitokeza kwanza kama msimulizi asiye mtendaji (anapotumia nafsi ya tatu kusimulia) anaposema: "Mchungaji mwenzake alisema" (Sabuni, 2008:13). Baada ya maelezo hayo, msimulizi anabadilika kutoka msimulizi asiye mtendaji na kuwa msimulizi mtendaji anapojivika uhusika wa mchungaji wa awali na kusema: "…Ingawaje kuna mila potofu pia. Hii ya maalbino kunyanyapaliwa ina dosari. Siyo mila ya kuachwa iendelee hata kidogo" (Sabuni, 2008:13). Kupitia kauli hiyo ya mchungaji, tunauona uhusika wa msimulizi ni hai kwa kuwa anajibainisha kwa kutumia nafsi ya kwanza na ya pili, ikimaanisha msimulizi anazungumza na msomaji wake kwa kumpa maelekezo au maagizo "siyo mila ya kuachwa iendelee hata kidogo" (Sabuni, 2008:13). Kwa hiyo, msimulizi anakosoa mila potofu zilizopo katika jamii hasa hii ya kuamini kuwa, viungo vya watu wenye ualbino vina nguvu za kichawi zinazomwezesha mtu kutajirika. Kwa hivyo, msimulizi katika bunilizi ya *Zindera* anahitimisha dhima

ya kukosoa kwa kusema kuwa, "…siyo mila ya kuachwa iendelee hata kidogo" (Sabuni, 2008:13).

Mtazamo uliopo katika jamii unaojitokeza kupitia dhima ya ukosoaji ni wa kisasa kwa sababu msimulizi anatusimulia kuhusu tabia ya baadhi ya watu wanaoua watu wenye ualbino kwa ajili ya kutafuta mali, utajiri na vyeo. Mtazamo huu umejidhihirisha kupitia mazungumzo ya wachungaji ambao walikuwa wanauliza kwa nini watu wanadanganywa na wanakubali kudanganyika.

Dhima ya msimulizi kama mkosoaji si ngeni kwani hata katika fasihi zingine duniani imebainika kuwapo pia. Mathalani, msimulizi katika riwaya ya *Bartleby The Scrivener* ya Helman Melville (1853) anaelezea kuhusu hadithi ya *Wall Street,* ambapo msimulizi anatueleza kuhusu mhusika Bartleby ambaye ameamua kuacha kufanya kazi ofisini kwake na kuamua kukaa kijiweni palipojulikana kama *Wall Street.* Msimulizi anamkosoa kwa kitendo hicho anachokifanya (Enotes, 2018).

### 5.2 Kueleza Itikadi

Itikadi ni mfumo wa mawazo ambao unatumika kuongoza jamii kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Itikadi ya jamii fulani inaweza kudhihirika kupitia mitazamo fulani wanayoifuata katika jamii ikiwemo haki za binadamu, imani kwa kutaja chache. Dhima hii ya kueleza itikadi inajitokeza katika bunilizi hii ya *Zindera* katika simulizi ya mzee Makale na mke wake hawakujaliwa kupata mtoto maishani mwao, na kwa bahati wanamwokota Zindera msituni. Msimulizi anasema hivi:

> Makale alikuwa na mkewe, ambapo kwa miaka yote waliyoishi pamoja hawakubarikiwa kupata mtoto. Katika ukoo wao, maalbino hawakuwa na kasoro. Walihesabiwa kama binadamu wengine. "Hatimaye Mola amenijaalia," Makale alisema. "Nitamtunza mtoto huyu kwa nguvu zangu zote. Endapo mwenyewe atatokea, basi nitamkabidhi (Sabuni, 2008:16).

Msimulizi anajitokeza kupitia msimulizi asiye mtendaji (kwa sababu anatumia nafsi ya tatu kusimulia) anaposimulia kuhusu familia ya Makale na mkewe, ambao walikuwa na tatizo la kukosa mtoto yaani walikuwa na tatizo la utasa na ugumba. Kutokana na hali hiyo, wanandoa hawa walitamani japo wapate mtoto na ilikuwa sababu mojawapo ya kamchukua Pili (ambaye hakuwa na wazazi) ili wakae naye kama mtoto wao. Msimulizi katika nukuu hiyo anatumia neno

"hawakubarikiwa". Neno hili linatudokeza kwamba watoto ni baraka anayopewa mtu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, msimulizi hapa si mtendaji (kwa sababu hajitokezi kwa nafsi ya kwanza au ya pili) bali anajitokeza kwa nafsi ya tatu anapotuandaa kufahamu kuhusu mazingira ya kuokotwa Zindera na kupelekwa nyumbani kwa Makale na mkewe.

Msimulizi anabadilika kuwa msimulizi asiye mtendaji na kuwa msimulizi mtendaji pale anapojivika uhusika wa Makale kwa kusema maneno yanayoashiria amepata baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu; ni baraka ya kumpatia mtoto aliyemwokota msituni.

Vilevile, kupitia simulizi kati ya Sundi ambaye ni kijakazi wa Bitele na Zindera, tunaona pia dhima ya itikadi ikijitokeza. Dhima hii inajitokeza kutokana na tukio la kuwaua watu wenye ualbino linalofanywa na Bitele ambaye ni mganga wa kienyeji. Msimulizi katika kitabu cha watoto cha *Zindera* anajitokeza kupitia msimulizi asiye mtendaji anaposema: "Sundi, msichana mtumishi wa Bitele alielewa kila kilichoendelea. Kwa miaka mingi, aliishi kwa Bitele. Mara nyingi alishuhudia mauaji ya maalbino" (Sabuni, 2008:39). Msimulizi anatujengea taharuki kwanza kabla hatujasikia anachokisema kuhusu suala hili. Msimulizi katika muktadha huu yuko tuli. Kisha msimulizi anabadilika uhusika wake wa msimulizi asiye mtendaji na anakuwa msimulizi mtendaji pale anapojivika uhusika wa Sundi na kusema; "Namuonea huruma sana msichana huyu…" (Sabuni, 2008:39). Maneno haya ambayo Sundi anazungumza mwenyewe na nafsi yake, yanamfanya msimulizi awe hai katika simulizi hii. Msimulizi yuko hai kutokana na kujitokeza kwa nafsi ya kwanza anaposema "Namuonea huruma" ikimaanisha msimulizi anashiriki katika usimulizi.

Dhima hii ya itikadi inatuonesha suala la kuthamini utu kupitia kauli ya Sundi ambaye alifahamu fika kuhusu jambo ambalo lingempata Zindera baada ya kufikishwa kwa mganga wa kienyeji. Kauli ya Sundi isemayo, "siwezi kumwacha aangamie" (Sabuni, 2008:39) inaonesha thamani ya uhai wa mtu. Sundi amethamini uhai wa Zindera ambao ulikuwa utolewe na wauaji wawili waliotumwa na Bitele kwa ajili ya Mage mteja wake. Kwa hiyo, tunapata dhima ya itikadi katika simulizi.

Mtazamo unaojitokeza hapa kuhusu watu wenye ualbino ni wa kisasa kwa sababu unahusisha mauaji ya watu wenye ualbino kwa sababu ya kupata mali, utajiri na vyeo. Tunaona msimulizi anaibua itikadi mbalimbali zikiwemo za masuala ya kujali utu na kuheshimu haki za binadamu, ambazo kwa ujumla wake zinapinga vikali vitendo vya mauaji ya binadamu.

Dhima hii ya itikadi si ngeni katika fasihi mbalimbali duniani ikiwamo fasihi ya Kimarekani. Msimulizi katika riwaya ya Ralph Ellison (1952) inayoitwa *Invisible Man* anasimulia kuhusu kijana ambaye ni Mmarekani Mweusi na rangi yake inamfanya asionekane katika jamii. Inahusiana na suala la ubaguzi wa rangi katika jamii ya Kimarekani ambapo watu weusi walibaguliwa katika kuzipata haki zao. Msimulizi anajitokeza kwa dhima ya itikadi akikosoa baadhi ya mambo yaliyokuwa yanafanywa kinyume na utu na ubinadamu (SparkNotes, 2017).

**5.3 Kusimulia**

Katika bunilizi ya *Zindera,* msimulizi anatusimulia kuhusu ndoa ya Sara na Mpanduji ilivyokuwa ya furaha, wifi zake Sara pamoja na mama mkwe walimpenda mno. Ili kudhihirisha jambo hili msimulizi anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji (yaani anayetumia nafsi ya tatu kusimulia) ili kutujengea taharuki kuhusu uhusiano wa mke na mume ulivyoanza, yaani jinsi walivyokuwa wanapendana. Msimulizi anasema hivi: "Sara aliolewa na Mpanduji. Baada ya sherehe kubwa, familia hii ilianza maisha katika kijiji cha Igake" (Sabuni, 2008:1). Msimulizi anabadilika nafasi yake kutoka kuwa msimulizi asiye mtendaji (msimulizi asiye hai) na anakuwa msimulizi mtendaji (msimulizi hai) anapojitokeza kama Mpanduji kwa upande mmoja na kama Sara kwa upande mwingine kutokana na majibizano watakayoyafanya. Msimulizi anasema yafuatayo: "Huu ni wakati wa furaha kubwa… Nimepata mke ninayempenda sana" (Sabuni, 2008:1). Hapo msimulizi ni mtendaji kwa kuwa anahusika moja kwa moja kusema anachokisema kwa kutumia nafsi ya kwanza. Kisha Sara anajibu: "Furaha ipo kwetu sote … Sikushawishiwa na mtu kukupenda. Naamini ndoa yetu itadumu" (Sabuni, 2008:1). Hapo pia msimulizi ni mtendaji kutokana na kutumia nafsi ya kwanza kusimulia maneno ya Sara. Dhima ya msimulizi ni hai katika simulizi hii kwa kuwa anatimiza majukumu kadhaa kama mhusika kutokana na matumizi ya nafsi ya kwanza. Pia, msimulizi na msomaji wanashirikiana kusimulia hadithi kutokana na matumizi ya nafsi ya pili inapotumika katika simulizi. Matumizi ya nafsi ya pili ni katika mazungumzo kama ilivyojitokeza kati ya mume na mke hapo juu.

Msimulizi anabadilika tena na kuwa msimulizi asiye mtendaji anaposema, "Awali hapakutokea tatizo lolote katika familia hiyo. Mama yake Mpanduji alimpenda sana Sara" (Sabuni, 2008:1). Baada ya msimulizi kujitokeza kama msimulizi asiye mtendaji anabadilika na kuwa msimulizi mtendaji anapovaa uhusika wa mama mkwe wa Sara pamoja na wifi yake Sara kama anavyosema:

"Nimepata mkwe mwema sana"…"Nami nimepata wifi mzuri"… "Natamani kumtembelea kila mara" (Sabuni, 2008:1). Nafasi hii ya msimulizi mtendaji (yaani anayatimiza majukumu) inabadilika tena na kuwa msimulizi asiye mtendaji (yaani msimulizi asiyetimiza makujumu bali ni mtazamaji) kutokana na kutumia nafsi ya tatu kusimulia. Kubadilikabadilika huku kwa uhusika wa msimulizi kunatueleza kuhusu mambo anayoyaunga mkono na asiyoyaunga mkono. Katika mambo anayoyaunga mkono anajitokeza kama msimulizi mtendaji ambaye dhima yake inakuwa ni hai. Lakini katika mambo ambayo hayaungi mkono, msimulizi anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji na dhima yake inakuwa ni tuli (si hai) ikimaanisha kuwa hayaungi mkono mambo yanayosemwa.

Dhima ya kusimulia inajitokeza pia kuhusiana na simulizi ya kuwasili kwa mtoto mchanga duniani kunajitokeza kwa namna inayomfanya mama mzazi wa mtoto huyu aone aibu na kutamani kuuficha uso wake kwa mumewe. Msimulizi anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji anapotujengea mazingira ya kujifungua kwa Sara. Msimulizi anaijenga taharuki hiyo kwa kusema yafuatayo: "…Mtoto mchanga aliwasili duniani. Hisia kali za mkunga Nzeta zilikuwa kwa aina ya mtoto aliyezaliwa" (Sabuni, 2008 :4). Katika muktadha huu, msimulizi siyo mtendaji kwa sababu anatumia nafsi ya tatu kusimulia, kwa hiyo yeye ni mtazamaji. Lakini baada ya msimulizi kutoa kauli hiyo, anabadilisha uhusika wake na kuwa msimulizi ambaye ni mtendaji anapojivika uhusika wa mkunga Nzeta na kusema yafuatayo: "Masikini…Ni kitoto cha kike lakini albino" (Sabuni, 2008 :4). Kitendo cha mhusika kujipambanua kwa kutumia nafsi ya kwanza kinatueleza kuhusu uhusika wake katika simulizi kwamba na yeye ni mhusika mtendaji. Lakini pia tunafahamu kuwa dhima yake ni hai katika muktadha huo.

Baada ya kauli hiyo ya mkunga kutolewa, msimulizi anabadilisha tena uhusika wake na kuwa msimulizi asiye mtendaji anapotushirikisha fadhaa iliyomshika Sara, ambaye ni mama wa mtoto baada ya taarifa hiyo kutolewa. Msimulizi anasema: "Sara aliguna. Mapigo ya moyo wake yaliongezeka mara dufu. Hata katika baridi wakati huo wa mvua, Sara alitokwa na jasho" (Sabuni, 2008:5). Katika muktadha huu, msimulizi amejitokeza kama msimulizi asiye mtendaji kutokana na kutumia nafsi ya tatu kusimulia jambo linalotupeleka kwenye tafsiri kwamba amejitenga na simulizi. Pia, tafsiri inayojitokeza hapo ni ya msimulizi tuli yaani hayuko hai katika usimuliaji wa simulizi hiyo. Kisha msimulizi anatushirikisha kuhusu huzuni ya Sara baada ya kuona mwitikio wa

mkunga na hapo msimulizi anabadilisha tena uhusika wake na kujivika uhusika wa kiutendaji anapovaa sura ya Sara na kusema: "Albino!" Sara aliongea kwa huzuni. "Albino, albino kabisa!" Akaangua kilio akasema, "Nitamwambia nini mume wangu? Nitauficha wapi uso wangu lakini siyo kitu" (Sabuni, 2008 :5). Kwa hivyo, uhusika wa msimulizi umebadilika tena kutoka msimulizi mtendaji na kuwa msimulizi asiye mtendaji ambaye anatujulisha kuhusu kilio cha Sara, na mara anabadilisha tena uhusika wake na kuwa msimulizi mtendaji (kwa kuwa anatumia nafsi ya kwanza kusimulia) akijivisha uhusika wa Sara na kutoa kauli yake ya kujipa moyo kwa kusema "lakini siyo kitu". Kubadilika huku kwa uhusika wa msimulizi kunatueleza kuhusu mambo anayoyaunga mkono kwa kuwa anayasimulia kupitia nafsi ya kwanza (anakuwa na dhima hai) na yale asiyoyaunga mkono pale anapoyasimulia kwa kutumia nafsi ya tatu, jambo linalotudhihirishia kuwa yanayozungumzwa hakubaliani nayo.

Si hivyo tu, bali dhima hii ya kusimulia pia inajitokeza pale msimulizi anapotusimulia kuhusu ziara ya Sara na mtoto wake mchanga kwa mume wake ili kumwonesha mtoto wao aliyemzaa; japo Sara mwenyewe alishitushwa na aina ya mtoto huyo. Msimulizi anapozungumzia hayo anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji (kwa sababu ya matumizi ya nafsi ya tatu) anapotuandaa kufahamu nini kitatokea pale Mpanduji ambaye ni baba wa mtoto mchanga aliyezaliwa atakapofahamu mwanawe ni mwenye ualbino. Msimulizi anasema hivi, "Sara alifika kwa mumewe wakati jua linazama. Mumewe alijawa na furaha akampokea mtoto aliyefunikwa blanketi" (Sabuni, 2008:5). Hapa msimulizi siyo mtendaji kwa kuwa hashiriki kusimulia, bali ni mtazamaji anayeiangalia simulizi kwa nje. Mara msimulizi anabadilika uhusika wake na kuwa msimulizi ambaye ni mtendaji (kutokana na matumizi ya nafsi ya kwanza) anapojivika uhusika wa Sara na Mpanduji kwa kusema yafuatayo, "Ni wa kike," Sara alisema. "Ni bahati ilioje?" Mpanduji alisema kwa furaha (Sabuni, 2008 :5). Kwa hiyo, hapa msimulizi ni mtendaji kwa kuwa anatimiza majukumu katika simulizi kupitia nafsi ya kwanza ya usimulizi. Hivyo, dhima ya msimulizi ni hai kutokana na uhusika wake ni wa kitendaji zaidi. Msimulizi kuwa hai inamaanisha anaunga mkono simulizi inayotolewa. Lakini kadri mazungumzo ya Sara na Mpanduji yanavyoendelea ndivyo uhusika wa msimulizi unavyojitokeza kwa namna tofautitofauti kwa sababu anaacha kuwa msimulizi mtendaji na sasa anakuwa msimulizi asiye mtendaji anapotupatia mazingira yaliyofuatia baada ya Mpanduji kufahamishwa kuwa mtoto ni wa kike. Msimulizi anasema hivi, "Akampokea mtoto na taratibu akamfunua blanketi" (Sabuni, 2008 :5). Katika mazingira haya

ya tukio hilo la Mpanduji kumpokea mtoto wake mikononi mwake linaelezewa kwa kutumia nafsi ya tatu ikimaanisha ni msimulizi asiye mtendaji ambaye anasimulia akiwa nje ya simulizi. Uhusika wake unabadilika tena na kuwa msimulizi mtendaji anapojivika uhusika wa Mpanduji na Sara na kuingia kwenye majibizano kama ifuatavyo: "He! ... Je, ni kitu gani hiki?" "Ni mtoto," Sara alisema. "Mwanao." "Hapana" (Sabuni, 2008:5). Msimulizi ameendelea kuwa na uhusika wa msimulizi mtendaji anaposema: "Albino!" Akamdondosha chini. "Mume wangu," Sara alisema, "yaani unakidondosha kiumbe! Je, humtaki mtoto huyu?" "Kabisa" (Sabuni, 2008:5). Kupitia mazungumzo hayo na majibizano kati ya Sara na mume wake, msimulizi anabadilikabadilika kiutendaji, mara anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji (anapotumia nafsi ya tatu kusimulia) mara anajitokeza kama mhusika mtendaji (anapotumia nafsi ya kwanza kusimulia anapojivika sura ya Mpanduji au Sara). Hii ni kwa sababu kuna wakati na yeye anashiriki katika simulizi na kuna wakati anajiondoa akibakia na dhima ya kusimulia tu bila kushiriki. Katika muktadha huo wa kusimulia kwa kutumia nafsi ya tatu - yeye ni mtazamaji.

Mtoto aliyezaliwa anaamua hatima ya ndoa ya Sara na Mpanduji kwa kuwa sasa Mpanduji ambaye alikiri kuwa anampenda sana mkewe, alikuwa tayari kuivunja ndoa hiyo iwapo Sara hatakubali kutengana na mwanawe. Msimulizi anasema, "Ni juu yako," alisisitiza. "Endapo utabaki uwe peke yako. Siyo na mwanao. Vinginevyo wewe na mwanao muondoke" (Sabuni, 2008 :5). Katika muktadha huu msimulizi amebadilisha uhusika wake na kuacha kuwa msimulizi asiye mtendaji (ambaye anasimulia yanayotokea) na kuwa msimulizi mtendaji (ambaye amevaa uhusika wa Mpanduji na kuzungumza yale yaliyoujaza moyo wake). Msimulizi anatumia nafsi ya pili, ikimaanisha anazungumza na msomaji kwa kumshirikisha naye atimize majukumu fulani. Kwa hiyo, dhima ya msimulizi katika muktadha huu ni hai kwa kuwa yeye na msomaji wanashirikiana katika kusimulia hadithi hii.

Kuvunjika kwa ndoa kati ya Sara na Mpanduji kunamfanya Sara atoroke na mtoto wake mchanga na kutokana na adha za safari hiyo, Sara anamficha Zindera msituni na hatimaye anaokotwa na mwindaji mmoja aliyefahamika kwa jina la Makale. Msimulizi anajitokeza kwa uhusika wa msimulizi asiye mtendaji anaposema: "Mwindaji Makale aliwasili nyumbani kwake. Mkewe, Bi. Sangi alitokwa na macho, akamshangaa mumewe" (Sabuni, 2008:16). Katika sehemu hii, msimulizi anatuandaa kufahamu nini kitazungumzwa na mke wa Makale pale atakapoona mumewe amekwenda na kichanga. Msimulizi kupitia Bi. Sungi

anasema: "Je, umeamua kuiba mtoto kwa sababu mimi ni mgumba?" (Sabuni, 2008:16). Makale anajibu: "Hapana… Hii ni bahati yetu sote. Mtoto huyo alitelekezwa msituni. Ni albino, tutamtunza milele" (Sabuni, 2008:17). Uhusika wa msimulizi umebadilika kutoka kuwa msimulizi asiye mtendaji (yaani anayesimulia kinachotokea kwa kutumia nafsi ya tatu) na kuwa msimulizi mtendaji anayehusika katika hadithi kutokana na kujivika uhusika wa Bi. Sungi na Bwana Makale na hivyo kutumia nafsi ya kwanza na ya pili katika majadiliano kati yao.

Kupitia kauli zao, msimulizi anabadili hata mwelekeo wa simulizi kwani mwanzoni alishiriki kutaka kumuua mtoto aliyezaliwa na ualbino (hapa alikuwa anatekeleza mtazamo wa kwanza wa kuwaua watu wenye ualbino kutokana na imani potofu); lakini sasa msimulizi amebadilika kimtazamo na amekuwa mwokozi. Msimulizi mtendaji amekuwa mwokozi kwani amemlinda Zindera asishambuliwe na wanyama wakali mwituni kwa upande mmoja; lakini kwa upande wa pili, amemfanya Bwana Makale "awe na utu" wa kumwokota Zindera na kumnusuru uhai wake. Kwa hiyo, kuokotwa kwa Zindera kunamaanisha kutengana na mama yake kwa maana kila mmoja atakwenda kusikojulikana. Kutengana kwa mama na mtoto, kunamwezesha mama wa mtoto (Sara) kuanza ukurasa mpya wa maisha bila mwanawe akiwa katika mji wa ugenini. Katika muktadha huo, msimulizi anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji kwani kazi yake ni kusimulia tu anaposema, "Sara alisimulia kisa chake bila woga. Vile alivyoolewa kwa furaha, akajifungua albino na hata kutoroka kwake" (Sabuni, 2008 :21). Msimulizi anabadilika tena dhima na kuwa msimulizi mtendaji anapovaa uhusika wa Sara kama ifuatavyo: "Sikuwa na njia nyingine…Nililazimika kumficha mwanangu msituni" (Sabuni, 2008:21).

Kwa hiyo, msimulizi anabadilika kimtazamo na kuonekana kuwa yeye ni kiumbe mwenye utu na huruma. Tunayaona haya kupitia mhusika Joshi anaposema: "Je, hatuwezi kumwokoa?" (Sabuni, 2008 :21). Kwa hiyo, msimulizi amebadilika kutoka kuwa muuaji na sasa anataka kuwa mwokoaji ili akamwokoe Zindera baada ya kuarifiwa kuwa amefichwa msituni. Hivyo, Sara akapokelewa na kuwa sehemu ya familia ya Bwana na Bibi Joshi. Nyota ya Sara inaanza kung'ara anapokutanishwa na mtoto mkubwa wa kiume wa Joshi ambaye ni polisi huko mjini. Mtoto huyo wa Mzee Joshi anaitwa Afande Pita. Wazazi wa Afande Pita wanamsifia Sara kwa kijana wao wakionesha wamemuunga mkono wazo la kijana wao la kumuoa Sara. Katika mazingira hayo, msimulizi anajitokeza kwa dhima ya msimulizi asiye mtendaji anaposimulia. Lakini mara

anabadilisha uhusika wake na kuwa msimulizi mtendaji anapovaa uhusika wa Afande Pita na vilevile uhusika wa wazazi wake Afande Pita kama asemavyo hapa: "Ni msichana imara." Joshi alisema. "Mchapakazi. Mcheshi. Mpole na anayehitaji kufarijiwa kutokana na mkasa uliompata" (Sabuni, 2008:27). Kwa hiyo, hapa msimulizi anajitokeza kwa uhusika wa msimulizi asiye mtendaji kutokana na matumizi ya nafsi ya tatu ambayo yanamfanya msimulizi awe mtazamaji tu. Uhusika wa msimulizi asiye mtendaji unabadilika na kuwa msimulizi mtendaji anapojivika uhusika wa Afande Pita na kusema: "Huyu atafaa kuwa mke wangu" (Sabuni, 2008:27). Hapa msimulizi anajitokeza kwa dhima hai kwa kuwa anatumia nafsi ya kwanza kusimulia na pia anatenda majukumu kadhaa katika simulizi.

Baada ya mazungumzo hayo, msimulizi anabadilika uhusika wake na kuwa msimulizi asiye mtendaji anapotuandaa kupata mrejesho wa wazazi wake Afande Pita baada ya kueleza nia yake ya kumwoa Sara. Msimulizi anasema hivi: "Wazazi wake walifurahia uamuzi huo. Hata Sara hakuwa na kipingamizi" (Sabuni, 2008:27). Kupitia kubadilikabadilika huku kwa uhusika, msimulizi anabadilika kimtazamo na kihisia kwa kuwa, sasa anataka kumrejeshea tena Sara furaha yake ya mume ambayo msimulizi pale mwanzoni alimwondolea. Siku zilivyozidi kusonga mbele Sara aliendelea kufaidi maisha yake mapya ya ndoa huku mwanawe Zindera akikumbana na mkasa wa kufiwa na wazazi wake wapenzi (walezi) Bwana Makale na mkewe Bi. Sungi, waliofariki kwa ajali ya moto. Kutokana na hilo, Zindera anakosa mtu wa kumlipia karo na hivyo anaanza kufunga safari ya kumtafuta shangazi yake ili amsomeshe.

Msimulizi anajitokeza kama msimulizi mtendaji anapojivika uhusika wa Mage, mtu anayeonekana kumhurumia Zindera kwa kumuuliza: "mwanangu unatafuta nini huku porini?" Msimulizi anaendeleza uhusika huu wa msimulizi mtendaji kupitia Zindera anapojibu: "nina shida kubwa…na sina mtu wa kunilipia karo ya shule." "Ingia garini. Nitakupeleka Bongoi…endapo utamkosa, nitajitolea kukusomesha" (Sabuni, 2008:37-38). Msimulizi kupitia mazungumzo haya, anajitokeza kama msimulizi mtendaji ambaye ameificha siri ya Mage kuhusu lifti ile aliyompatia Zindera. Msimulizi ameificha siri ya Mage kuhusu huruma aliyomwonesha Zindera kwa kumwita "mwanangu", jambo lililomfanya Zindera amwamini na kumwona ni mtu mwenye nia njema kwake. Jambo hili la kusimulia kwa kutumia nafsi ya kwanza linatueleza kwamba msimulizi ni mtendaji. Pia, msimulizi anaunga mkono yanayosimuliwa kwa sababu matumizi ya nafsi ya kwanza yanamaanisha uungaji mkono. Vilevile, kitendo hiki

kitadhihirisha kuwa msimulizi yuko hai kwenye simulizi hii. Msimulizi anabadilisha mwelekeo wa kisimulizi anapoacha kuwa msimulizi mtendaji na kuwa msimulizi asiye mtendaji pale anapotusimulia kuhusu mikasa inayompata Zindera tangu apewe lifti na Mage na kujikuta yuko mikononi mwa wauaji wa watu wenye ualbino. Hatimaye Zindera anatoroka na kujikuta anapokelewa katika familia mpya. Msimulizi anajitokeza kama msimulizi asiye mtendaji kwa sababu anatuandaa kisaikolojia kuhusu mapokezi ya Zindera katika nyumba ya Sara. Baada ya Sara kueleza kuwa alikuwa na mtoto aliyeitwa Zindera lakini aliuawa na mume wake, msimulizi anasema haya: "Zindera alicheka akasema" (Sabuni, 2008:54). Hapa msimulizi siyo mtendaji kwa kuwa yuko nje ya simulizi. Yuko nje ya simulizi kwa sababu anatumia nafsi ya tatu ili kusimulia hadithi. Jambo hili linatueleza kuhusu umbali uliopo kati ya msimulizi na simulizi husika.

Baada ya msimulizi kutuandaa hivyo kisaikolojia, uhusika wa msimulizi unabadilika na sasa anakuwa msimulizi mtendaji anapojitokeza kama Zindera ambaye anamfariji Sara kuhusu Zindera wake aliyeuawa kwa kusema: "Ni bahati kubwa sana. Ulikuwa na mtoto aliyeitwa Zindera. Kwa bahati mbaya huna tena Zindera. Zindera mwingine alizaliwa sasa, amekua na amekoswakoswa kuuawa na watu wakatili. Huyu, unaye sasa hivi. Punguza machungu juu ya Zindera aliyetoweka. Mimi nipo hapa kwa ajili yako. Ni Zindera mpya" (Sabuni, 2008:54). Hapa msimulizi ni hai kwa kuwa na yeye yuko ndani ya simulizi akisimulia hadithi hii. Msimulizi yuko ndani kwa kuwa anatumia nafsi ya kwanza na nafsi ya pili ili kusimulia hadithi. Jambo hili litatupa tafsiri kwamba dhima ya msimulizi katika usimulizi ni hai kwa sababu naye anatimiza majukumu kadha wa kadha kama mhusika Sara au mhusika Zindera.

Kisha uhusika wa msimulizi unabadilika kutoka kuwa msimulizi mtendaji na kuwa msimulizi asiye mtendaji anaposema: "Sara alisema huku tabasamu limempamba uso wake" (Sabuni, 2008:54). Kitendo hicho cha msimulizi kusimulia kwa nafsi ya tatu kinamaanisha amejitenga na simulizi na yeye siyo sehemu ya hayo yanayoongelewa. Dhima yake ya kiusimulizi ni tuli. Baada ya kauli hiyo ya Sara, msimulizi anarudia tena uhusika wa awali wa msimulizi mtendaji akijivika uhusika wa Sara na kusema: "Hii ni faraja ya pekee. Pole sana na masaibu yaliyokukuta" (Sabuni, 2008:54). Hapa msimulizi ni hai kutokana na matumizi ya nafsi ya kwanza yanayomfanya awe mtendaji katika simulizi na siyo mtazamaji. Kupitia kauli hiyo, msimulizi anabadilika tena uhusika huo na kuwa msimulizi asiye mtendaji ambaye anaendelea kumwandaa msomaji kuhusu maisha mapya ya Zindera katika familia ya Afande Pita na mkewe Sara kwamba

Zindera anaendelea kukua kimwili na kiakili ambapo Afande Pita anachukua jukumu la kumsomesha kama mwanawe. Zindera anafanikiwa kimasomo na anahitimu chuo kikuu na kuwa tabibu. Kupitia kazi yake hiyo, anakutana na Mpanduji kama mmojawapo wa wagonjwa ambaye baada ya kumtibu na kukosa ndugu wa kumwangalia, Zindera anaamua kumkaribisha nyumbani kwao ili akae na familia yake ambayo ni ya Afande Pita, Sara, Pili (msichana aliyemlea Zindera alipokuwa ameokotwa) pamoja na Zindera mwenyewe. Kupitia familia hii mpya yenye watu watano, Zindera anaweka bayana ndoto zake na uhusika wa msimulizi unaendelea kuwa msimulizi asiye mtendaji katika muktadha huu msimulizi si hai kwa kuwa yuko nje ya simulizi kama mtazamaji.

Kisha msimulizi anajitokeza kwa uhusika wa msimulizi mtendaji anapojivika uhusika wa Zindera na kutuelezea ndoto zake kuhusu kutetea watu wenye ualbino. Msimulizi anasema: “nikiwa bungeni nitalinda na kutetea haki za maalbino wote” (Sabuni, 2008:67). Kupitia jibu la Afande Pita, msimulizi anaendelea pia kuwa msimulizi mtendaji anaposema: “unaweza kuwa mbunge…tayari jina lako ni maarufu hapa kwetu. Endelea na ujasiri wako” (Sabuni, 2008:67). Zindera anatiwa moyo na baba yake ambaye ni Afande Pita kuhusu juhudi pamoja na mipango yake. Msimulizi kupitia baba yake Zindera (Afande Pita) anataja neno “ujasiri” kwa maana bila “ujasiri” vita dhidi ya imani potofu za mauaji ya watu wenye ualbino ni ndoto kuitimiza. Unahitajika “ujasiri” wa hali ya juu ili kukabiliana na wadau wa biashara hiyo.

Kutokana na mazungumzo haya kati ya Zindera na Afande Pita, tunamwona jinsi ambavyo msimulizi amebadilika hata mtazamo. Msimulizi ameweza kubadilisha imani aliyokuwa nayo ya kuwaua watu wenye ualbino wanapozaliwa, “huu ni mkosi katika familia” (maneno ya Mpanduji ambaye ni baba yake mzazi Zindera) - kauli ambayo inaakisi mtazamo wa kwanza wa imani potofu za kuwaua watoto wanaozaliwa na ualbino na sasa anafikiria kuwatetea na kuwalinda ili wasiuawe tena, anaposema: “nitalinda na kutetea maalbino wote” (Sabuni, 2008:67). Kwa hiyo, msimulizi amebadilika kwa maana sasa amekuwa mwerevu na ameondokana na tatizo la ujinga uliokuwa umemgubika fikra zake. Dhima ya msimulizi ni hai kwa kuwa anatimiza majukumu yake ya kiusimulizi kwa kuvaa uhusika wa Zindera na kusimulia kwa nafsi ya kwanza. Maana ya matumizi hayo ya nafsi ya kwanza yanaonesha kuwa msimulizi yuko karibu na simulizi pia dhima yake ni hai. Baada ya msimulizi kujitokeza kama msimulizi mtendaji ghafla anabadilisha uhusika wake na kujitokeza kama msimulizi asiye mtendaji pale anapoelezea hisia za Zindera kama ifuatavyo:

"Zindera alitabasamu kwa muda bila kuongea. Sara na Mpanduji walitazamana. Pili alikunywa maji taratibu…Kukawa na shangwe kubwa kwa kujumuika wote pale sebuleni" (Sabuni, 2008:68). Kwa hiyo, msimulizi amebadilisha uhusika wake kwa kuacha kuwa msimulizi mtendaji na sasa amekuwa msimulizi asiye mtendaji na lengo ni kuonesha nafasi yake ni ya utazamaji zaidi (mtazamaji) na siyo mtendaji (mhusika anayetimiza majukumu katika simulizi).

Mtazamo unaojitokeza hapa kuhusu watu wenye ualbino ni wa kisasa kwa sababu unahusisha mauaji ya watu wenye ualbino kwa sababu ya kupata mali, utajiri na vyeo. Tunaona msimulizi anasimulia jinsi Zindera alivyokoswakoswa kuuawa kwa sababu mganga alitaka kumuua ili apate viungo vya binadamu kwa ajili ya kutengeneza dawa za kuwapatisha watu utajiri na kuwapandisha vyeo.

### 5.4 Kuwasiliana

Dhima ya kuwasiliana imejitokeza kupitia mazungumzo kati ya mume na mke baada ya Mzee Makale kuokota kichanga msituni na kwenda nacho nyumbani kwake. Msimulizi kupitia Bi. Sungi anasema: "Je, umeamua kuiba mtoto kwa sababu mimi ni mgumba?" (Sabuni, 2008:16). Makale anajibu: "Hapana… Hii ni bahati yetu sote. Mtoto huyo alitelekezwa msituni. Ni albino, tutamtunza milele" (Sabuni, 2008:17). Uhusika wa msimulizi umebadilika kutoka kuwa msimulizi asiye mtendaji (yaani anayesimulia kinachotokea kwa kutumia nafsi ya tatu kuhusu namna Makale alivyookota mtoto msituni na kisha kwenda naye nyumbani kwake) na kuwa msimulizi mtendaji (anayehusika katika hadithi kutokana na kujivika uhusika wa Bi. Sungi na Bwana Makale) kupita mazungumzo kati yao ambapo wanatumia nafsi ya kwanza na ya pili katika majadiliano kati yao. Kinachoelezwa hapa kinashadidia dhima ya mawasiliano kutokana na mazungumzo ambayo wahusika wanayafanya baina yao. Kule kuzungumza na kujibizana ndiko kunakofanya dhima hii ijitokeze kwa kuwa nafsi ya kwanza na ya pili inajitokeza katika matumizi na siyo nafsi ya tatu.

Mtazamo unaojitokeza hapa kuhusu watu wenye ualbino ni wa kizamani kwa sababu unahusisha mauaji ya watu wenye ualbino kwa sababu ya kuzaliwa na hali hiyo. Tunaona msimulizi anaibua mtazamo huo kupitia dhima ya kuwasiliana na tunalijua hili baada ya kuokotwa Zindera msituni, baada ya kutupwa na wazazi wake wakiogopa kupata mikosi na mabalaa.

## 6.0 Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa kuchambua dhima mbalimbali za msimulizi zinazotumika kusimulia hadithi ya ualbino katika kazi teule ya bunilizi ya watoto ya *Zindera*. Tumeweza kubaini dhima za aina nne ambazo ni: kukosoa, kueleza itikadi, kusimulia, na kuwasiliana. Kwa kupitia Nadharia ya Naratolojia, tumebaini kwamba, msimulizi anaweza kujitokeza kwa dhima tofauti na siyo ya kusimulia pekee, japokuwa hiyo ndiyo dhima inayotawala katika kazi hii teule tuliyoichambua.

Utafiti umebaini kuwa, msimulizi anapotekeleza dhima ya itikadi, anajitokeza kwa nafsi ya kwanza ya wingi au nafsi ya kwanza ya umoja. Matumizi ya nafsi ya kwanza umoja yanamaanisha msimulizi anataka kutushirikisha uzoefu wake wa maisha pamoja na tajiriba. Pia matumizi ya nafsi ya kwanza yanamaanisha msimulizi anakubaliana na hoja au mawazo yanayoongelewa katika simulizi na hivyo anayaunga mkono. Vilevile, matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yanamaanisha kuwa msimulizi anazungumza na jamii nzima kama sehemu inayohusishwa na itikadi hizo, na hivyo anasisitiza mabadiliko au mageuzi.

Kwa upande mwingine, msimulizi anapotimiza dhima ya kukosoa amejitokeza kwa nafsi ya tatu ikirejelea watu wengine ambao wana tabia au mawazo ambayo msimulizi hayaungi mkono. Hii inaweza kufasiriwa kuwa, watu huona kasoro kwa watu wengine na siyo kuziona kasoro zao wenyewe; na kutokana na hilo ndipo dhima ya kuwakosoa wengine inapojitokeza. Matumizi ya nafsi ya tatu yanamaanisha kwamba msimulizi hayaungi mkono maneno au hoja zinazoongelewa na hivyo amejitenga na simulizi.

Vilevile, msimulizi amejitokeza kwa nafsi ya pili anapotekeleza dhima ya mawasiliano ambapo anazungumza na msomaji. Hii ni kwa sababu kazi ya nafsi ya pili ni kuonesha kuwa msimulizi anazungumza na msomaji wake. Matumizi ya nafsi ya pili yanamaanisha kwamba msimulizi anataka kumhusisha msomaji katika kutekeleza majukumu ya kuisimulia hadithi.

Utafiti umebaini pia, msimulizi anapotekeleza dhima ya kuwasiliana na itikadi anakuwa hai zaidi kwa sababu anatumia nafsi ya pili na ya kwanza ili kukamilisha dhima hizo. Lakini kwa upande mwingine, msimulizi anapotekeleza dhima ya kukosoa na kusimulia anakuwa si hai yaani tuli kwa kuwa anakuwa ni mtazamaji na siyo mtendaji na hivyo anatumia nafsi ya tatu. Kwa hiyo, katika utafiti huu, tumeweza kuona kuwa, msimulizi ana dhima hai na dhima tuli katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali.

Kwa kuongezea, utafiti umebaini kuwa usimulizi unapotumia nafsi ya tatu unaakisi uhalisia wa mambo katika jamii. Ni uhalisia kuhusiana na mambo yanayotendeka dhidi ya watu wenye ualbino. Kwa mujibu wa data yetu ya utafiti, uhalisia unajitokeza dhima ya msimulizi inapokuwa tuli, ikimaanisha kuwa, yeye si sehemu ya simulizi bali ni mtazamaji.

Vilevile, utafiti umebaini kuwa, msimulizi anapotumia nafsi ya kwanza (kama ni umoja au wingi) ndipo anaposhughulikia mambo yanayohusiana na ualbino kiyakinifu. Uyakinifu unajitokeza pale msimulizi anapokuwa ndani ya simulizi ambayo inamaanisha hajajitenga na usimulizi. Dhima ya msimulizi ni hai kwa kuwa na yeye anahusika katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Kwa hiyo, uchambuzi huu wa matumizi ya sauti za usimulizi umeweka bayana kwamba ni wakati gani msimulizi anajihusisha na simulizi (yaani anaunga mkono yanayosemwa) na wakati gani anajitenga nayo (yaani haungi mkono yanayosemwa). Hivyo, uchambuzi huu umetuwezesha kuona jinsi uhusika wa msimulizi unavyobadilika kwa kuwa na dhima hai au dhima tuli na pia kuwa msimulizi mtendaji au msimulizi asiye mtendaji na tumeweza kufahamu sababu anuai za ujitokezaji huo kama zilivyojadiliwa katika uchambuzi wetu.

Utafiti wetu umebaini kuwapo kwa aina zote mbili za mitazamo inayojitokeza kuhusu watu wenye ualbino. Mtazamo wa kuua watoto wenye ualbino pale wanapozaliwa ili kuondokona na mikosi, mabalaa na nuksi. Mtazamo wa pili ni kuua watu wenye ualbino kwa ajili ya kupanda vyeo na kupata mali na utajiri. Mtazamo wa kizamani unajitokeza kupitia dhima ya kusimulia ambapo mtoto Zindera baada ya kuzaliwa alikusudiwa auawe na baba yake mzazi na hatimaye akatupwa msituni. Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisasa umejitokeza kupitia dhima ya kukosoa, kuibua itikadi mbalimbali pamoja na kusimulia. Katika dhima hii msimulizi anaibua mtazamo huo kupitia mauaji ya watu wenye ualbino kwa ajili ya kupata utajiri na vyeo.

## Marejeleo

Altman, R. (2008). *A Theory of Narrative Structure.* New York: Columbia University Press.

Bal, M. (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative.* 2nd edition. Toronto: University of Toronto Press.

Bonn, A. (2014, October 23). *Role of Narrator in American Novel*. Katika https://study.com/academy/lesson/role-of-the-narrator-in-american-novels-types-and-examples.html. Imesomwa Januari 10, 2019.

Boyd, N. (2015, May 4). *Role of the Narrator in British Novel Types & Examples.* katika http://study.com. Imesomwa Februari 2, 2019.

Bordwell, D. (1985). *Narration in the Fiction Film*. Madson: University of Wisconsin Press.

Coles, W.H. (2018). *Ist Person POV in Literary Story*. Katika http://www.storyinliteraryfiction.com. Imesomwa Januari 10, 2019.

Enotes (2015, February 21). *Bartleby the Scriver, A Tale of Wall Street.* Katika http://www.enotes.com. Imesomwa Machi 10, 2019.

Fludernik, M. (2006). *An Introduction to Narratology.* London: Routledge.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay on Method.* Trans. Jane E. Lewin. Ithaca: Cornell University Press.

Hubert, H.W. (2016). Assessing the Role of the Narrator in The Verse Novel: A Look at Pushkni's Eugene Onegin. (Tasinifu ya Umahiri). University of Ghana.

Jann, M. (2005). *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative.* Cologne: English Department, University of Cologne.

Madumulla, J.S (2009). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limied.

Mahenge, E. (2019). Uuumbaji wa Ualbino katika Fasihi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Kazi Teule. Tasinifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Matt, D. (2003). "The Influence of Narrative Tense in Second Person Narration: A Response to Joshua Parker." *Connotations*. 23(1): 55-62.

Mohochi, E.S. (2000). "Usimulizi wa Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*." *Nordic Journal of African Studies*. 9(2): 49 - 59.

Phelan, J. (2005). *Living To Tell about It*. Ithaca: Cornell University Press.

Prudchenko, K. (2017). Pen the Pad: The Difference Between an Observer and a Participant in a Narrative. Katika http://penandthepad.com. Imesomwa Januari 10, 2019.

Schmidt, J.N. (2014). Narration in Film – the living handbook of narratology. wikis.sub.uni-hamburg.de. Imesomwa Februari 10, 2019.

SparkNotes. (2018, August 24). *Invisible Man.* m.sparknotes.com Imesomwa Februari 10, 2019.

Surber, K. (2015, June 29). *First Person Narrator Definition & Example.* http://study.com. Iimesomwa Juni 10, 2019.

Tendler, A. (2012, October 8). *Passive Vs. Active: The Role of the Narrator – Literature Technology*. Katika www.briancroxall.net. Imesomwa Juni 10, 2019.

Walsh, R. (1997). "Who is Narrator?" *Poetics Today*. 18(4), 495-513. Katika http://www.jstor.com/stable/1773184. Imesomwa Julai 10, 2019.

Wiehardt, G. (2018, July 18). *Second – Person Point of View*. Katika http://www.thebalancecareers.com. Imesomwa Julai 10, 2019.